

TANGAZO



15.03.2023

TANGAZO LA MAOMBI YA VIBANDA KATIKA ENEO LA STENDI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale anawatangazia wananchi wote wakiwemo watu **binafsi, Kampuni/Makampuni, Taasisi, Kikundi/Vikundi** kutuma maombi ya kupanga kwenye vibanda vilivyojengwa na Halmashauri katika eneo la stendi ya Liwale. **Namba ya Zabuni LGA/054/2022/2023/NC/01.**

MASHARTI YA JUMLA YA MAOMBI

1. Mwombaji awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
2. Ada ya maombi ni **TZS 20,000/=** ambayo haitarudishwa (**non-refundable fee**). Ada zote za maombi zitalipwa kwenye akaunti ya Halmashauri kupitia ofisi ya mweka hazina ambapo mwombaji atapatiwa **Control Number ya malipo** inayopatikana katika Ofisi ya Mweka Hazina (W), barua ya maombi ni sharti iambatane na **risti ya malipo**.
3. Mwombaji wa biashara ya bucha ni lazima awe na mashine za kisasa za kukatia nyama.
4. Mwombaji awe tayari kuweka mita ya umeme ambayo itasajiliwa kwa jina la Halmashauri na gharama zake zitarejeshwa kwa makubaliano ya makato ya pango hadi deni litakapoisha.
5. Mwombaji aombe kibanda anachotaka kupanga kwa kuandika namba ya banda husika kwenye barua yake ya maombi.
6. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri.
7. Mwombaji aeleze kiasi cha pango anachoweza kuilipa Halmashauri kwa mwezi.
8. Mwombaji awe tayari kulipa kodi ya kila mwezi bila usumbufu.
9. Mwombaji awe tayari kuingia mkataba na Halmashauri kwa masharti yatakayowekwa na Halmashauri.
10. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **30.03.2023** Saa **9:30** Alasiri.
11. Maombi yote yatumwe kwa anwani ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale; ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA LIWALE
S.L.P 23, LIWALE